# THE TIMER NATIONAL EXAMINATIONS
# K C P FIRST TRIAL 2022

**DARASA LA NANE**
**KISWAHILI**
**SEHEMU YA KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

## SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

## JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**16.** Chagua zana ya kivita ambayo si ya kisasa.

A. Kifaru
B. Manati
C. Nyambizi
D. Manowari

Jibu sahihi ni **B (Manati)**

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 16, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

[6] A B C D [16] A B C D [26] A B C D [36] A B C D [46] A B C D

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Mwanafunzi aangalie ya kuwa maswali yote kwenye kitabu yamepiga chapa.

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.**

Katika baadhi ya ____1____ humu nchini, tatizo la uhaba wa maji ____2____ kuwaka kama____3____. Wakazi wa maeneo hayo ____4____ changamoto kwani bei ya maji nayo imepanda maradufu. Wanaochuuza maji mitaani kwa ____5____nao hawana ____6____ kwani ____7____ wakazi wa maeneo hayo na ____8____, wamepandisha bei ya bidhaa hiyo muhimu bila chembe ya hisia.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. magatuzi | B. gatuzi | C. mataifa | D. mabara |
| 2. | A. yanaendelea | B. inaanza | C. linaendelea | D. unazidi |
| 3. | A. jua la mtikati | B. moto wa kifuu | C. hasira za mkizi | D. upepo wa tufani |
| 4. | A. wamekumbwa | B. wamekumbana | C. wamekumba | D. wamekumbwa na |
| 5. | A. mkokoteni | B. manowari | C. rukwama | D. helikopta |
| 6. | A. amani | B. mioyo | C. shukrani | D. imani |
| 7. | A. hawahurumii | B. hawawahurumii | C. hawawahurumi | D. hawahurumi |
| 8. | A. badala yake | B.baada yake | C. kabla yake | D. mahali pake |

Elimu ina ladha yake. Ingawa haihisiki kwa ulimi, utamu upo. ____9____. Nasema hivi kwa sababu nimeyaona manufaa ya elimu. Nina uwezo wa kutambua maradhi kama ____10____ambayo huambukizwa na ____11____ na mashairi ya aina nyingi kama vile ____12____ ambapo mshororo wa tano hukamilisha kila ____13____. Licha ya hayo, nimewafahamu wafanyakazi mbalimbali. ____14____ kuwa mfanyakazi anayeshughulikia mitambo ndiye ____15____.

**9.** A. Ukiujua huu na huu huujui — B. Elimu ni taa, gizani huzagaa — C. Aisifuye mvua imemnyea — D. Msema pweke hakosi

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. malaria | B. malale | C. UKIMWI | D. Korona |
| **11.** | A. chawa | B. kukohoa | C. ngono | D. mbung'o |
| **12.** | A. takhmisa | B. tarbia | C. tathlitha | D. tathmina |
| **13.** | A. mizani | B. ubeti | C. kina | D. ukwapi |
| **14.** | A. Ninamjua | B. Namjua | C. Ninafahamu | D. Ninamfahamu |
| **15.** | A. mwandishi | B. mhandisi | C. injini | D. sogora |

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu swali kulingana na maagizo.***

16. Chagua sentensi yenye tanakali ya sauti.
A. Lo! Kumbe alikuwa shangazi yake!
B. Wanafunzi walisoma kutwa kucha.
C. Sarafu ilianguka mchangani tifu!
D. Baba wa Juma ni mkali kama simba.

17. Chagua kiwakilishi katika sentensi hii.
**Kijana huyu ni mzuri kushinda yule.**
A. yule B. mzuri
C. huyu D. kushinda

18. Tumia kirejeshi **amba** badala ya o-rejeshi.
**Wanafunzi waliofuzu vizuri walizawidiwa.**
A. Wanafunzi ambao waliofuzu vizuri walizawidiwa.
B. Wanafunzi ambao walifuzu vizuri walizawidiwa.
C. Wanafunzi ambaye walifuzu vizuri walizawidiwa.
D. Wanafunzi ambayo walifuzu vizuri walizawidiwa.

19. Kamilisha methali:
**Mwana wa kuku hafunzwi**
A. kuriaria B. kutembea
C. kuchakura D. kupuruka

20. Chagua majina yaliyo katika ngeli ya YA-YA pekee.
A. Maumbo, maktaba, mate.
B. Makawa, matatu, maji.
C. Maradhi, maskanini, makavazi.
D. Mafuta, mazingira, mauti.

21. Ni neno gani halijaambatanishwa ipasavyo na jibu lake?
A. Buriani inshallah.
B. Makiwa tunayo
C. Alamsiki binuru
D. Sabalkheri aheri

22. Chagua sentensi iliyotumia o-rejeshi tamati kwa usahihi.
A. Wageni wanaokuja ni wetu.
B. Wanafunzi watakaotutumbuiza waje hapa mbele.
C. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.
D. Waliotuzwa wawape nafasi wengine watuzwe.

23. Chagua sentensi sahihi kutokana na maneno haya:
**Kitabu, cha, nipe, vitate, hiki**
A. Nipe vitate cha hiki kitabu.
B. Kitabu hiki cha vitate nipe.
C. Nipe hiki kitabu cha vitate.
D. Nipe kitabu hiki cha vitate.

24. **Makia ya mabuzi haya ni mafupi** katika wastani ni
A. mkia wa mbuzi huyu ni mfupi.
B. mikia ya mbuzi hawa ni mifupi.
C. mikia ya mbuzi hao ni wafupi.
D. mkia wa mbuzi huyo ni mfupi.

25. Ni ipi ala ya muziki kati ya maneno yafuatayo?
A. Parapanda B. Manati
C. Manowari D. Nyambizi

26. Kanusha:
**Ningeenda ningempata akipepeta pojo kwenye ungo.**
A. Singeenda singempata akipepeta pojo kwenye ungo.
B. Nisingeenda singempata akipepeta pojo kwenye ungo.
C. Nisingeenda nisingempata akipepeta pojo kwenye ungo.
D. Nisingeenda nisingepata akipepeta pojo kwenye ungo.

27. Tegua kitendawili.
**Wanashindana wakifuatana.**
A. Kufuli B. Samaki
C. Mtu na kivuli D. Magurudumu

28. Chagua jibu linaloonyesha sifa iliyoundwa kutokana na nomino.
A. Saka msasi
B. Ushujaa shujaa
C. Cheza mchezo
D. Lipa malipo

29. Chagua neno lenye sauti changamano.
A. Mtoto B. Watoto
C. Mwavuli D. Wayo

30. Upi ni usemi halisi wa sentensi ifuatayo?
**Maono alisema kuwa alikuwa akiwachukia waliowaajiri watoto.**
A. Maono alisema, "ninawachukia wanaowaajiri watoto.
B. Maono alisema, "Ninawachukia wanaowaajiri watoto."
C. Maono alisema, mimi siwapendi wanaowaajiri watoto.
D. Maono alisema anawachukia wanaowaajiri watoto.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Ajali za barabarani nchini zimeongezeka maradufu. Swali ni je, nani aelekezewe kidole cha lawama? Ni serikali, ni madereva au ni sisi wasafiri? Hiki kimebaki kitendawili kisichoweza kuteguliwa. Kila siku utasikia kutoka kwenye vyombo vya habari watu walioaga dunia kutokana na ajali. Hili ni jambo la kuatua moyo hasa kwa wale wanaofiwa na wapenzi wao katika ajali.

Mojawapo ya kiini cha ajali barabarani kwetu ni barabara mbovu. Barabara zilizoharibika huchangia pakubwa katika kusababisha ajali. Mashimo yaliyojaa barabarani hufanya magari kuyumbayumba na kisha kupoteza mwelekeo. Mwishowe magari hugongana dafrau na hivyo kusababisha vifo vya watu wasiokuwa na hatia. Serikali yetu ina jukumu kubwa katika kukarabati barabara. Wawape kandarasi watu walio na ujuzi katika ujenzi wa barabara.

Vilevile, magari yanayobeba abiria kupita kiasi husababisha ajali. Dereva na kondakta wake huwasomba abiria ukadhani ni mashehena ya mizigo. Lengo la haya yote ni ulafi wa pesa. Lawama hapa zinafaa kuelekezwa kwa madereva, makondakta na abiria. Ni sharti wenye magari wajali masilahi ya wasafiri, nao wasafiri ningewashauri kutoabiri magari yaliyojaa abiria.

Isitoshe, magari mabovu katika barabara zetu pia ni chanzo cha ajali. Si ajabu kuwaona madereva wakiyaendesha makatara barabarani. Magari hayo huharibikia mahali popote na wakati wowote. Waendeshaji hawa hujipa moyo na kujitetea kwa methali isemayo **ukuukuu wa kamba si upya wa ukambaa**. Hatua thabiti za kisheria zinafaa kuchukuliwa na serikali ili kuyaondoa magari ya aina hii. Tukumbuke kuwa kinga ni bora kuliko tiba. Aidha, tutahadhari kabla ya hatari.

Fauka ya hayo, madereva wasiohitimu huchangia katika kusababisha ajali. Wao huendesha magari bila kuhitimu. Labda waliwahonga wanaohusika na utoaji wa leseni. Hawajui ishara za barabarani. Kwa mfano, kivuko cha watoto na hata wanyama, barabara zenye matuta na pengine ishara ya kuonyesha kuruba. Wanaotoa leseni wanapaswa kuwajibika na kutoshiriki ufisadi.

Madereva waliotumia dawa za kulevya pia husababisha ajali. Uwezo wao wa kuona vyema huathirika kwa sababu ya vileo. Wao hawamakiniki wanapoendesha magari. Mihadarati pia huwafanya wengine kuendesha magari kwa kasi mithili ya duma. Wao husahau kuwa haraka haraka haina baraka.

Ni sharti sote tuungane mikono ili kukomesha ajali katika barabara zetu. Tukumbuke kuwa nia zikiwa moja, kilicho mbali huja. Sisi ndisi wenye nchi na kumaliza ajali kunatutegemea sisi.

31. Katika aya ya kwanza, ni nani anastahili kulaumiwa kutokana na ajali?

A. Madereva B. Abiria

C. Hafahamiki D. Serikali

32. Ni orodha ipi iliyo na vyombo vya habari **pekee**?

A. Redio, televisheni, tishali.

B. Gazeti, redio, televisheni.

C. Majarida, kiyoyozi, redio.

D. Runinga, uyoka, magazeti.

33. Barabara zilizoharibika husababishaje ajali?

A. Magari huendeshwa kwa kasi na baadaye kuyumba.

B. Magari huharibika, kuyumbayumba na kugongana.

C. Magari hupoteza njia na kugongana.

D. Magari huyumbayumba na kuwagonga wapitanjia.

34. Kwa nini madereva huwabeba abiria kupita kiasi?

A. Mara nyingi wao huwa na haraka.

B. Abiria hupenda kubanana kama ndizi.

C. Wao huwa na tamaa ya pesa.

D. Viti huwa vichache mno magarini.

35. Ni nini maana ya methali <u>ukuukuu wa kamba si upya wa ukambaa</u>?

A. Tusidharau vitu vya zamani kwa kutamani vipya.

B. Vitu vya zamani huwa tofauti na vipya.

C. Tusividunishe vitu vipya kwani vina faida nyingi.

D. Vitu vya zamani huwa si vizuri kama vipya.

36. Madereva wasiohitimu huwezaje kupata leseni?

A. Huzinunua kutoka madukani.

B. Hupewa na maafisa wa trafiki barabarani.

C. Hutoa hongo.

D. Hupewa na serikali.

37. Kulingana na ufahamu, mihadarati husababisha haya yote **ila**

A. shida za kutazama barabarani.

B. madereva kuugua magonjwa yatokanayo na dawa za kulevya.

C. madereva kukosa uangalifu wanapoendesha magari.

D. magari kuendeshwa kwa kasi.

38. Unafikiri ni njia ipi mwafaka ya serikali kuhakikisha kuwa magari yameendeshwa kwa mwendo wa kadiri?

A. Kuwa na maafisa wa trafiki katika kila mji nchini.

B. Kuandaa semina kuwahamasisha abiria.

C. Magari kutiwa vidhibitimwendo.

D. Kutoa adhabu kali kwa abiria wanaoabiri magari yaliyojaa abiria.

39. Ni ushauri upi uliotolewa kwa wale wote wasababishao ajali?

A. Kuwafahamisha askari wa trafiki kasoro yoyote ya madereva.

B. Kutowahonga wanaotoa leseni.

C. Kutoabiri magari yaliyojaa wanaposafiri.

D. Kuchukua tahadhari wanaposafiri.

40. Kichwa kinachofaa **zaidi** ufahamu huu ni kipi?

A. Athari za ajali barabarani.

B. Chanzo cha ajali barabarani.

C. Njia za kuzuia ajali barabarani.

D. Ufisadi katika sekta ya uchukuzi.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Vumilia alikuwa mtoto wa kike. Alikuwa **kifunguamimba** katika familia ya mzee Juhudi. Baba wa Vumilia alikuwa maskini wa mali lakini tajiri wa moyo. Alifanya kazi za kijungujiko kuwakimu wanawe na mkewe ambaye walichukuana kama sahani na kawa. Wazee wa Vumilia walikula yamini kufanya kila waliloweza ili kumrithisha mwana wao ufunguo wa maisha.

Vumilia alipohitimu darasa la nane, wazazi wake walichochea ari yake ya kufuzu maishani kwa kutumia mifano halisi ambayo Vumilia aliielewa. Wazee hao walimkumbusha binti yao kuwa bidii, utiifu, uvumilivu pamoja na heshima na uadilifu zilikuwa siri kubwa ya fanaka. Naam! Ilibainika kuwa **samaki hukunjwa angali mbichi.**

Binti wa watu alipopasuliwa mbarika, alikuwa kama mbwa aliyeonyeshwa ufuko, akakataa abadan katan kufa maji. Aliongeza bidii maradufu katika masomo yake na kuwa kama anayetegemea kisomo kuishi. Waliosema kuwa bidii hulipa hawakukosea. Mtihani ulipofanywa na matokeo kutolewa, Vumilia aliwaacha wengi vinywa wazi kwa kuwa alikuwa amewashinda watahiniwa wote nchini.

Halikuwa la mjadala tena. Anayechovya asali hachovyi mara moja. Vumilia hakulegeza kamba wala kuangalia nyuma. Makini yake yalikwama masomoni. Licha ya kuwa kijana, alikataa kuwa bendera ya kufuata upepo. Alimakinikia ndoto yake ya kuwa mhasibu ili kuwaauni wazee wake kama njia ya kushukuru kwa yote waliyoyatenda. Wafadhili wake waliridhishwa na hatua yao ya kumfadhili Vumilia tangu shule ya msingi hadi chuo kikuu.

Hewaa! Hayawi hayawi huwa. Tunapozungumza sasa, Vumilia ni mhasibu mkuu katika benki kuu ya Tulizeni. **Amewajengea wazee wake kasri** na kuhakikisha kuwa wanapata kila wanalohitaji. Daima huwasomesha wadogo wake na kuwahimiza kufanya bidii za duduvule wakifahamu mno kuwa jasho la leo ndilo faraja ya kesho.

41. Ni kweli kusema kuwa katika familia ya mzee Juhudi,
A. Vumilia alikuwa mtoto wa pekee.
B. Vumilia alikuwa yatima aliyefadhiliwa.
C. kulikuwa na watoto kadhaa.
D. Vumilia hakuwa na wanuna wowote.

42. **<u>Kifunguamimba</u>** ni sawa na
A. mwanambee.
B. ndugu mdogo.
C. mtoto wa pekee.
D. mtoto wa mwisho.

43. Wazazi wa Vumilia waliichochea ari yake
A. alipokuwa katika shule ya msingi.
B. baada ya kumaliza masomo ya sekondari.
C. alipokuwa katika chuo kikuu.
D. alipomaliza masomo ya msingi.

44. Ni sifa gani ambayo wazazi wa Vumilia hawakumfunza kama siri ya fanaka?
A. Bidii.
B. Utiifu.
C. Ujanja.
D. Uadilifu.

45. Katika kidokezi **<u>samaki hukunjwa angali mbichi</u>**, anayelinganishwa na samaki hapa ni
A. vumilia.
B. wazazi.
C. walimu.
D. wanuna wa Vumilia.

46. Kilichomwezesha Vumilia kupita vizuri katika mtihani wa darasa la nane ni
A. utajiri wa wazazi wake.
B. hali ya umaskini wao.
C. ushauri wa wazazi wake.
D. mtihani kuwa rahisi.

47. Vumilia alikuwa tofauti na vijana wenzake kwa kuwa
A. hakushawishika kufuata mkondo mbovu.
B. aliamua kuwa mhasibu.
C. alisoma hadi chuo kikuu.
D. aliwafaa wazaziwe baadaye.

48. **<u>Amewajengea wazee wake kasri</u>** ni
A. nahau.
B. tanakali ya sauti.
C. istiara.
D. tashbihi.

49. Wafadhili wa Vumilia
A. walijutia uamuzi wao.
B. walimwonea fahari Vumilia.
C. walimwonea wivu Vumilia.
D. walisikitikia mafanikio ya Vumilia.

50. Methali gani inayoweza kutumiwa kufupishia ujumbe wa ufahamu huu?
A. Heri nusu shari kuliko shari kamili.
B. Mali bila daftari hupotea bila habari.
C. Hasara humpata mwenye mabezo.
D. Mvumilivu hula mbivu.